



Simu: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imepanga kupokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 (The Finance Bill, 2026)** kwa mujibu wa Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Mkutano wa kupokea na kusikiliza maoni ya wadau (Public Hearing) utafanyika kuanzia siku ya **Jumamosi tarehe 20 Juni** hadi **Jumapili tarehe 21 Juni, 2026 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa**, Bungeni Jijini Dodoma.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huo, Kamati inawaalika wadau wote kufika kwenye Mkutano huo na kuwasilisha maoni yao kabla haujapelekwa katika hatua nyingine.

Aidha, maoni yanaweza pia kuwasilishwa kwa njia ya posta kupitia anuani ya Ofisi ya Bunge au kupitia Barua pepe ya [**cna@bunge.go.tz**](mailto:cna@bunge.go.tz) na [**kamati@bunge.go.tz**](mailto:kamati@bunge.go.tz).

Muswada huo unaweza kupakuliwa katika Tovuti ya Bunge [**https://www.parliament.go.tz/bills-list**](https://www.parliament.go.tz/bills-list).

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.

19 Juni, 2026.

